**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06** **URAIA NA MAADILI**

**Muda: Saa 1:30** **SULUHISHO** **Mwaka: 2022**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B zenye jumla ya maswali **sita (06)**
2. Jibu maswali **yote**


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org

***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

SEHEMU A (Alama 26)

1. Jibu vipengele (i) – (v)

(i) Mtu anayetekeleza majukumu yake ipasavyo anajulikana kama:
A. msikivu
B. mtiifu
C. mwaminifu
D. mwajibikaji
**Jibu: D. mwajibikaji**
Sababu: Mtu anayejua majukumu yake na kuyatimiza kwa usahihi anaitwa mwajibikaji.

(ii) Lipi ni mojawapo ya jukumu la mtoto katika familia?
A. Kuheshimiwa na familia
B. Kupendwa na familia
C. Kusikilizwa na familia
D. Kujali mali za familia
**Jibu: D. Kujali mali za familia**
Sababu: Kujali mali za familia ni jukumu la mtoto kuhakikisha haziharibiki.

(iii) Vitendo vifuatavyo vinaonesha jinsi watu wanavyothamini rasilimali zetu isipokuwa:
A. Kupanda miti
B. Kulinda wanyamapori
C. Kuchoma misitu
D. Kutunza vyanzo vya maji
**Jibu: C. Kuchoma misitu**
Sababu: Kuchoma misitu ni tendo la uharibifu wa mazingira, si utunzaji.

(iv) Watu wanaotembea pembeni mwa barabara hujulikana kama:
A. Madereva
B. Polisi wa Trafiki
C. Waenda kwa miguu
D. Wamachinga
**Jibu: C. Waenda kwa miguu**
Sababu: Watu wanaotembea kwa miguu kwenye barabara ni waenda kwa miguu.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***

(v) Ni shughuli ipi ya kujitolea kati ya hizi mtoto anaweza kuifanya katika jamii?
A. Kuchimba na kujenga barabara
B. Kuotesha na kutunza miti
C. Kuchimba na kuuza madini
D. Kununua na kuuza maji
**Jibu: B. Kuotesha na kutunza miti**
Sababu: Kuotesha na kutunza miti ni shughuli ya kujitolea inayosaidia jamii.

2. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha majukumu ya viongozi wa wanafunzi katika Kifungu A na vyeo vyao katika Kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi

(i) Mwanafunzi anayefuatilia ufundishaji na ujifunzaji shuleni
**Jibu: E. Kiranja wa Taaluma**

(ii) Mwanafunzi anayesimamia majukumu yote ya viranja shuleni
**Jibu: C. Kiranja Mkuu**

(iii) Mwanafunzi anayehakikisha wanafunzi wanaingia darasani na kuwa na tabia njema
**Jibu: D. Kiranja wa nidhamu**

(iv) Mwanafunzi anayehakikisha kuwa shule inavutia na kupendeza muda wote
**Jibu: F. Kiranja wa usafi**

3. Jibu vipengele (i) – (ii) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kutatua changamoto hutusaidia (kufikia malengo yetu, kufanya kazi kwa bidii, kuwa maarufu)
**Jibu: kufikia malengo yetu**
Sababu: Kutatua changamoto kunasaidia mtu kufanikisha malengo yake.

(ii) Mwanafuzi mwenye tabia nzuri ni yule ambaye ___________________
(kufanya kazi mwenyewe tu, kushirikiana na wenzake, kusaidia walimu tu)
**Jibu: kushirikiana na wenzake**
Sababu: Ushirikiano unaonyesha tabia nzuri na ufanisi katika kazi.

(iii) Mawazo mazuri au mabaya aliyonayo mtu juu ya jambo fulani huitwa?
**Jibu: mtazamo**
Sababu: Mtazamo ni maoni au mitazamo mtu anayo nayo kuhusu jambo fulani.

(iv) Watu wa dini tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa Amani endapo: (watalazimishana kufuata dini moja, watawafukuza watu wasio na dini, wataheshimiana)
**Jibu: wataheshimiana**
Sababu: Kuheshimiana ndio msingi wa amani kati ya watu wa dini tofauti.

4. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuonesha matendo ya utunzaji wa mazingira na matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama (√) kwenye tendo husika

i) Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji
**Uharibifu wa Mazingira:** √

ii) Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima
**Utunzaji wa Mazingira:** √

iii) Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng'ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa
**Uharibifu wa Mazingira:** √

iv) Mzee Daudi ameotesha miti kisha anakata mti mmoja kwa ajili ya mbao
**Uharibifu wa Mazingira:** √

5. Angalia kwa makini picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

(a) Taja matendo mawili yanayoonekana katika picha.
i) Wanafunzi wanashiriki katika michezo ya shule
ii) Wanafunzi wanajifunza kushirikiana katika shughuli za pamoja

(b) Ni wajibu gani ambao haujatimizwa na wazazi wa baadhi ya watoto wanaoonekana katika picha?
**Jibu:** Kuwapa watoto malezi sahihi na ushauri wa malezi

(c) Mara unapoona haki za mtoto zinakiukwa unatakiwa kufanya nini?
**Jibu:** Kuripoti tukio hilo kwa mwalimu au mamlaka inayohusika

(d) Kwanini kitendo kinachoonekana katika picha ya mtoto mwenye nyundo mkononi ni cha ukiukwaji wa haki za watoto?


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
*Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA*

**Jibu:** Kitendo hicho kinaonyesha kutumia vurugu badala ya elimu, hivyo haki za mtoto za usalama na mafunzo vinakiukwa

6. Soma kwa makini kifungu cha habari kinachofuata kisha jibu vipengele.

   Mawasiliano ni jambo la masingi na la lazima katika jamii yoyote, mathalani, hapo zamani watu walitumia njia za asili kuwasiliana na kupeana habari. Miongoni mwa njia hizo ni baragumu, ngoma, yowe na sauti mbalimbali za wanyama. Miaka ya hivi karibuni, njia za mawasiliano zimebadilika sana ambapo njia za kieletroniki hutumika kurahisisha mawasiliano baina ya watu. Miongoni mwa njia hizo za kisasa ni simu, runinga, barua pepe, magazeti na mitandao ya kijamii. Njia hizi za kisasa za mawasiliano ni sehemu ya utandawazi na zimeenea maeneo mengi duniani Utandawazi husadia masuala ya biashara, elimu, michezo n ahata siasa. Matumizi mazuri ya utandawazi huleta maendeleo kwa jamii. Matumizi mabaya ya utandawazi huweza kusababisha kupotea kwa maadili, kushuka kwa kiwango cha elimu n ahata yaweza kuwa chanzo cha kutoelewana kati yetu. Kwa hiyo, tunapaswa kutumia utandawazi vizuri kwa maendelo ya jamii yetu.

(a) Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma, taja njia mbili za kisasa za mawasiliano.
i) Simu
ii) Runinga

(b) Kwanini utandawazi ni muhimu katika jamii?
**Jibu:** Utandawazi unasaidia kueneza masuala ya biashara, elimu, michezo na siasa na kuleta maendeleo kwa jamii.

(c) Watu waliwasilianaje hapo zamani?
**Jibu:** Watu waliwasiliana kwa njia za asili kama baragumu, ngoma, yowe na sauti za wanyama.

(d) Kwanini tunapaswa kutumia utandawazi vizuri?
**Jibu:** Matumizi mazuri ya utandawazi huleta maendeleo, huku matumizi mabaya yakiweza kusababisha kupotea kwa maadili na kushuka kwa kiwango cha elimu.


Pata hii, pamoja na vitu vingine katika: https://maktaba.tetea.org
***Imeandaliwa na Maria Marco kwa TETEA***